# 4. Maria na Martha

**Luka 10:38-42**
**Mwanzo 3**
**Mada Muhimu: Ushirika na Bab**

[Dhana Muhimu za Injili: Urafiki wa karibu na Baba, Dhambi, Utambulisho katika Kristo]

**HADITHI:**

***Siku moja Yesu na wafuasi wake walikuwa wakisafiri, na wakafika katika kijiji kimoja ambapo mwanamke mmoja aliyeitwa Martha alimkaribisha nyumbani kwake. Martha alikuwa na dada yake aliyeitwa Maria. Maria aliketi chini miguuni mwa Yesu akisikiliza yale aliyokuwa akisema. Lakini Martha alikuwa akihangaika na maandalizi yote yaliyokuwa yafanyike. Martha kaja kwa Yesu akamuuliza, "Bwana, hujali kwamba dada yangu ameniachia kazi yote mwenyewe? Basi mwambie anisaidie!"***

***Lakini Bwana akamjibu, "Martha, Martha  mbona unasumbuka na kuhangaika na mengi? Lakini kunahitajika kitu kimoja tu. Maria amechagua kile kilicho bora, wala hakuna atakaye mwondolea"***

**AYA ya KUKUMBUSHA:**

- **Luka 10:42:** *"Kunahitajika kitu kimoja tu. Maria amechagua kile kilicho bora, wala hakuna atakayemwondolea."*

**SWALI LA UTANGULIZI** (Kujadili na jirani):

- **Mbona tunapaswa kuomba?**

**MPITO**

- Hadithi ya leo inatuambia kuhusu wanawake wawili waliomkaribisha Yesu nyumbani mwao, lakini walifanya hivyo kwa njia tofauti sana. Hebu tuangalie pamoja jinsi walivyokuja kwa Yesu.

**MJIFUNZE HADITHI PAMOJA (mazoezi ya kusikiliza)**

- **Maswali yanayoweza kukusaidia kusikiliza tunaporudia hadithi**
  - Mariamu alifanya maamuzi gani Yesu alipofika nyumbani kwake?
  - Martha alifanya maamuzi gani Yesu alipofika nyumbani kwake? Aliitikiaje uchaguzi wa Mariamu?

**MUHTASARI wa MSINGI wa Majadiliano** (kumsaidia mwezeshaji kuongoza bila kusoma kila kitu):

- **Martha:** Alikuwa mtu wa namna gani? Nini kilikuwa kizuri? Nini haikuwa nzuri? Je, alimtendeaje Yesu na dada yake? Ni nini kilikuwa muhimu zaidi kwake?
- **Mariamu:** Mtazamo wake kwa Yesu ulikuwaje? Ni nini kilikuwa muhimu zaidi kwake?
- **Yesu:** Aliitikiaje malalamiko ya Martha? Ni nini kilikuwa muhimu zaidi kwake?
- **Sisi:** Yesu anataka nini zaidi kutoka kwetu?
- **Kazi nzuri / nidhamu za kiroho:** Tunaweza kujifunza nini kutokana na hadithi hii?
- **Utekelezaji:** Ni nini kinachohitaji kubadilika katika maisha yangu baada ya kujifunza hadithi hii - baada ya kujifunza jinsi Yesu anataka tu tufurahie uwepo wake na kujifunza kutoka kwake? Ni matendo gani, mitazamo, au imani gani? Tunawezaje kuwapenda wengine vizuri zaidi?
- **Kushiriki:** Nani anahitaji kusikia hadithi hii?

## MASWALI ya MAJADILIANO

(pamoja na baadhi ya majibu yanayowezekana)

- **Martha alifanya nini wakati Yesu alikuja kijijini mwake? Alifanya nini wakati alikuja nyumbani mwake?**
- **Maria alifanya nini wakati Yesu alikuja ndani ya nyumba? Alikuwa wapi? Alikuwa na mtazamo upi kuhusu Yesu? Alifanya nini?**
- **Mbona Martha alikasirika? Alifanya nini kuhusu jambo hili? Jambo hili lilionyesha au fichua moyo wake unamna gani?**
  - *Martha alimkaribisha Yesu nyumbani kwake, lakini alikuwa akishughulika sana ili amfurahishe, hakufaulu kutulia na KUMJUA kwa undani na kumskiza. Martha alikuwa akihangaishwa na ile kazi ambayo alidhania ni muhimu kuitenda.*
- **Je, Martha alihangaikia nini zaidi? Unafikiri kwa nini alikuwa hivyo? Unafikiri ni nini kilichomfanya awe hivyo? Motisha wake ulikuwa upi?**
  - *Labda Martha alikuwa akijaribu kumvutia Yesu.*
  - *Martha alimfungulia Yesu nyumba yake lakini hakumfungulia Yesu moyo wake.*
  - *Alijishughulisha kumtumikia badala ya kumjua moyoni mwake.*
- **Maria likuwa akijishughulisha na nini zaidi? Mbona wafikiri alikuwa hivyo?**
  - *Alitaka kumjua Yesu, yaani kuketi katika uwepo wake.*
- **Yesu alijibu vipi kuhusu malalamiko ya Martha?**
  - *"Martha, Martha mbona unasumbuka na kuhangaika na mengi? Lakini kunahitajika kitu kimoja tu. Maria amechagua kile kilicho bora, wala hakuna atakaye mwondolea."*
- **Yesu alipoingia nyumbani (au maishani) ya mtu fulani alikusudia kufanya nini zaidi?**
  - *Kuwa na uhusiano naye*
- **Martha alimtenda Maria aje? Kwa nini? Tunaporuhusu kazi zetu "nzuri" zitutenganishe na tukose kuwa na Baba, jambo hili hufanya tuwatendee watu wengine vipi?**
  - *Inatufanya kuwa na kiburi, hasira, na wivu na watu wengine ambao tunafikiri hawafanya kazi kama sisi.*

- **Ni kwa njia gani Martha anafanana na Kaka Mkubwa katika hadithi ya Wana Wawili Waliopotea?**

- **Ikiwa mtu anaelewa na kuamini kile ambacho Yesu amemfanyia - kwamba alikufa msalabani na kufufuka kwa ajili yake - hiyo inawezaje kumsaidia kutamani kuwa na ushirika na Baba yake?**
  - *Ikiwa tunafikiri kwamba ni lazima tuendelee kupata kibali cha Mungu kupitia kazi zetu ngumu kwa ajili yake, tutaendelea kuwa na wasiwasi inapotokea kuwa vigumu au tunaposhindwa.*
  - *Ikiwa tunatumaini kikamilifu yale ambayo Yesu alitufanyia, tunaweza kustarehe nyakati fulani na kuchukua muda wa kuketi pamoja naye, bila kuhisi hatia kuhusu kazi yote tunayohitaji "kuzalisha" ili tujisikie vizuri.*
  - *Kuelewa msalaba kutatusaidia kuona kwamba Mungu anataka kuwa Baba yetu, anataka tuthamini uhusiano naye, anataka tuketi na kumsikiliza.*

**<u>MASWALI ya UTEKELEZAJI ya JUMLA</u>** (jadili na kikundi kizima)

- **Tunafananaje na Martha nyakati fulani?**
    - o *kutaka kuonekana mzuri mbele ya wengine, kuboresha au kudumisha sifa zetu*
    - o *kutaka kujisikia fahari, ujasiri, na haki mbele za Mungu*
    - o *tunajali sana kufanya wajibu wetu hivi kwamba hatuchukui muda wa kuketi na kumsikiliza Baba yetu anayetupenda.*

- **Je, ni baadhi ya mambo gani ya kawaida katika maisha yetu ambayo yanatukengeusha kutoka kwa kuketi kweli katika uwepo wa Baba?**

- **Ikiwa kumjua Yesu na kuwa pamoja naye mbele zake kukawa jambo la maana zaidi maishani mwetu, tunawezaje kuishi kwa njia tofauti? Je, mitazamo yetu ingekuwa tofauti vipi? Au matendo yetu? Je, tunawezaje kupunguza mwendo wa "kuketi" pamoja na kumsikiliza Yesu kutusaidia kuwapenda wengine?**

- **Ikiwa watu katika kanisa lako wangeanza kufikiria kumjua Yesu kuwa muhimu zaidi kuliko shughuli au mambo mengine yote, unafikiri kanisa lako lingekuwa tofauti na lilivyo sasa?**

**MASWALI ya UTEKELEZAJI ya KIBINAFSI** (chagua moja kwa majadiliano ya kikundi kidogo):

- **Can you think of a recent situation where you felt like Martha in this story? Perhaps a situation in your own life when you have failed to love others because of your busy work for the Lord?**

- **What works do you do "for the Lord"? How does this work, even though it is good, sometimes distract you from what is really needed - to be with your Father? What are you "worried and upset" about today? How can you repent of these distractions?**